TANGAZO LA SERIKALI NA. 29 la tarehe 17/02/2017

SHERIA NDOGO YA FEDHA YA SERIKALI ZA MITAA

(SURA 290)

# SHERIA NDOGO

*(Zimetungwa chini ya kifungu cha 7(1) na 16(1))*

SHERIA NDOGO ZA (ADA NA USHURU) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA NKASI ZA MWAKA 2017

## SEHEMU YA KWANZA

### UTANGULIZI

Jina na mwanzo wa kuanza kutumika

1. Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama Sheria Ndogo za (Ada na Ushuru) za Halmashauri ya Wilaya ya Nkasi za Mwaka 2017, na zitaanza kutumika mara baada ya kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali.

Matumizi

2. Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo lote lililo chini ya mamlaka ya Halmashauri ya Wilaya ya Nkasi.

Tafsiri

3. Katika Sheria Ndogo hizi isipokuwa pale itakapoelezwa vinginevyo:-

"Ada na Ushuru" maana yake ni malipo yanayolipwa kwa Halmashauri au Wakala wake kwa ajili ya huduma, vibali au leseni mbalimbali zitolewazo na Halmashauri.

"Afisa Muidhiniwa" maana yake ni Afisa yeyote wa Halmashauri aliyeteuliwa kusimamia Utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi.

"Biashara" maana yake ni shughuli yoyote halali inayofanywa na mtu, watu, taasisi, shirika au kampuni ya kuuza na kununua mazao na au bidhaa yoyote inayozalishwa ndani ya Halmashauri

"Chombo cha Usafiri" maana yake ni chombo chochote kinachotumika kusafirishia mtu, watu au mizigo kutoka sehemu

moja kwenda nyingine, bila kuhusisha mikokoteni na wanyama wanaotumika kusafirishia mizingo.

“Chombo cha Uvuvi” maana yake ni Mitumbwi, Boti au chombo kingine chochote kinachotumika katika shughuli za uvuvi.

“Doria” maana yake ni shughuli yoyote ya kushtukiza, kwa ajili ya kubaini na kukamata uharifu na waharifu.

“Halmashauri” maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Nkasi.

“Kibali/Leseni” maana yake ni idhini au ruhusa ya maandishi inayotolewa na Halmashauri.

“Kituo cha Mabasi/Stendi” maana yake ni eneo maalum lililotengwa na Halmashauri kwa lengo la kupakia na kutelemsha abiria na mizigo ya abiria.

“Machinjio” maana yake ni eneo lililotengwa na Halmashauri kwa ajili ya kuchinjia wanyama na kuanikia ngozi.

“Madini ya Ujenzi” maana yake ni kokoto, mawe, changarawe, mchanga, chokaa, malumalu, kifusi, udongo mfinyanzi au chochote kinachochimbwa kwa shughuli za ujenzi na kupatikana katika mamlaka ya Halmashauri.

“Mashine”maana yake ni nyenzo ya kielektroniki inayotumika katika biashara.

“Masoko” maana yake ni maeneo yoyote yaliyotengwa na Halmashauri kwa ajili ya kuuza na kununua bidhaa.

“Mazao” maana yake ni mazao yote yanayozalishwa kutoka mashambani, mistuni, majini na sehemu nyingine yoyote ndani ya Halmashauri.

“Mkurugenzi” maana yake ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Nkasi, na ni pamoja na Afisa yeyote wa umma atakayeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi.

"Mnada" maana yake ni sehemu maalum iliyotengwa na Halmashauri katika tarehe maalum kwa ajili ya kuendesha shughuli za kuuza na kununua bidhaa na Mifugo.

"Risiti" maana yake ni kielelezo cha maandishi kinachotolewa na Halmashauri au wakala kuonesha ufanyikaji wa biashara.

"Stakabadhi" maana yake ni hati maalum inayotolewa na Halmashauri kwa ajili ya malipo.

"Usajili" maana yake ni utaratibu wa kutambua na kuorodhesha kimaandishi mali, vyombo, mtu, taasisi, au namna yingine yoyote itakayoifanya Halmashauri kutambua uwepo wa kitu kilichosajiliwa.

"Wakala" maana yake ni mtu, Taasisi, Kampuni, au asasi yoyote iliyoteuliwa kisheria na Halmashauri kukusanya mapato ya Halmashauri kwa niaba yake

## SEHEMU YA PILI

### NAMNA YA KUKUSANYA ADA NA USHURU

Ada na Ushuru

4. (1) Halmashauri itatoza Ada na Ushuru mbalimbali kwa ajili ya Shughuli na huduma zitolewazo na Halmashauri kama inavyooneshwa kwenye jedwali la kwanza la Sheria Sheria Ndogo hizi.

(2) Ada na Ushuru utakaotozwa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi, utalipwa kabla ya huduma kutolewa.

(3) Bidhaa au huduma nyingine yoyote ambayo ilipaswa kutozwa ushuru ambayo haikutajwa na Sheria Ndogo hizi ambayo mtoza ushuru ataona kwa maslahi ya Halmashauri inafaa itozwe, itatozwa 5% ya bei ya soko la bidhaa hiyo kwa wakati huo.

(4) Ada na Ushuru utakaotozwa na Halmashauri utalipwa kwa Halmashauri au Wakala wake ambaye atatoa stakabadhi ya Malipo kwa mtoaji wa Ada na ushuru huo.

(5) Bila kuathiri kifungu kidogo cha 4 cha kifungu hiki cha Sheria Ndogo hizi, malipo yote yatafanyika kwa kutumia mfumo wa kielektroniki yaani I – tax au kwa mfumo wa kawaida wa stakabadhi za Halmashauri pale ambapo mfumo wa I – tax utakaposhindikana.

Maeneo ya kufanyia biashara

5. Mazao yote ndani ya Halmashauri yatauzwa katika maeneo maalum yaliyotengwa na Halmashauri kwa shughuli hiyo, na kwa mujibu wa Jedwali la Pili la Sheria Ndogo hizi.

Kulipa ada na ushuru.

6. 1) Itakuwa ni wajibu wa kila mtu anayetakiwa kulipa ada na Ushuru kuhakikisha kwamba analipa Ada na Ushuru kwa Viwango vilivyoainishwa na Sheria ndogo hizi.

(2) Muda wa kukusanya Ada na Ushuru utakuwa kuanzia saa kumi na mbili asubuhi mpaka saa kumi na mbili jioni.

(3) Muda wa kusafirisha Mazao au bidhaa yoyote inayotakiwa kulipiwa ushuru kwa Halmashauri itakuwa kuanzia saa 12.30 Asubuhi hadi saa 12.30 jioni.

(4) Malipo ya Ada na Ushuru yatafanyika kila siku au kwa muda maalum kulingana na makubaliano yatakayowekwa kati ya Halmashauri/wakala na mlipa Ada na Ushuru katika Mkataba kwa Mawakala.

(5) Malipo yote ya Ada na Ushuru yatalipwa kwa Halmashauri au wakala wake kwa mujibu wa Sheria ndogo hizi, na stakabadhi kama kielelezo cha malipo yaliyofanyika itatolewa.

Kibali cha kununua mazao

7. Mfanyabiashara anayetaka kununua mazao ndani ya Halmashauri atapashwa kupata kibali toka kwa Mkurugenzi, kama ilivyooneshwa katika jedwali la nne la Sheria Ndogo hizi.

Halmashauri kumteua wakala

8. Halmashauri ina mamlaka ya kumteua Mtu binafsi, Kampuni, Asasi, au Taasisi kukusanya Ada na Ushuru kwa Niaba yake.

Wakala kusimamiwa na Afisa Mtendaji kata

9. Kila Wakala atatakiwa kuripoti kwa Afisa Mtendaji wa Kata mahali uwakala wake ulipo, na Afisa Mtendaji huyo atakuwa na jukumu la kumsimamia wakala katika shughuli zake zote za ukusanyaji wa mapato ya Halmashauri na kuhakikisha kuwa anapata taarifa za Makusanyo ya kila, Miezi mitatu (3),sita (6), tisa (9) na Mwaka.

Waganga wa jadi kusajiliwa

10. Waganga wote wa jadi hawataruhusiwa kuendesha shughuli zao za uganga mpaka wawe wamesajiliwa kwa mujibu wa sharia ndogo hizi.

## SEHEMU YA TATU
## MAKOSA NA ADHABU

Makosa

11. Itakuwa ni kosa;

A. kwa Wakala

(a) Kukusanya Ada na Ushuru bila kibali cha maandishi au mkataba kutoka Halmashauri.

(b) Kujaribu au kukusanya Ada na Ushuru kwa kiwango tofauti na kilichotajwa katika Sheria Ndogo hizi.

(c) Kushindwa kuwasilisha au kuwasilisha kiwango pungufu cha Ada na Ushuru kilichokubaliwa katika mkataba.

(d) Kufanya uzembe au usumbufu wowote utakaoisababishia hasara Halmashauri iwe kwa kutokujua, kujua au kwa makusudi.

(e) Kuwaruhusu watumishi wake kuingia eneo la Halmashauri kukusanya Ada au ushuru bila kuvaa vitambulisho vya Wakala.

B. Kwa yeyote ambaye;-

(a) Atashindwa, atadharau, au kukaidi/kukataa kulipa Ada na Ushuru au kutotekeleza agizo lolote alilopewa na Halmashauri kuhusiana na ulipaji wa Ada na Ushuru chini ya Sheria Ndogo hizi.

(b) Atakimbia, ataharibu kizuizi au kufanya kitendo chochote kiovu kwa lengo la kukwepa kulipa Ada na Ushuru

(c) Atamshawishi mtu au kundi la watu kukataa au kukwepa kulipa Ada na Ushuru.

(d) Atatengeneza, atatayarisha, ataidhinisha utengenezaji au atatumia nyaraka za uongo Kwa nia ya kujipatia manufaa yatokanayo na ukusanyaji wa Ada na Ushuru mbalimbali ndani ya Halmashauri.

(e) Kwa maksudi atatoa taarifa za uongo kwa Halmashauri wakati akijua taarifa anazotoa ni za uongo au atashindwa kutoa taarifa zitakazohitajika na Halmashauri.

(f) Atashindwa kuweka kumbukumbu, vitabu, hesabu, au maelezo yoyote yatakayohitajika na Halmashauri.

(g) Kwa maksudi atasababisha au atapoteza nyaraka au sehemu ya nyaraka za Halmashauri, na

(h) Atamzuia Afisa Mwidhiniwa au Wakala kutekeleza majukumu yake.

Adhabu

12. Mtu yeyote atakayekwenda kinyume na masharti ya Sheria Ndogo hizi atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atatozwa faini isiyozidi shilingi elfu hamsini (50,000/=) au kifungo cha miezi sita jela au adhabu zote mbili kwa pamoja yaani faini na kifungo

Kufifi-lisha kosa

13. Mkurugenzi atakuwa na uwezo wa kumtoza faini mtu yeyote isiyozidi shilingi elfu hamsini (50,000/=) iwapo mkosaji atakiri kwa maandishi kutenda kosa hilo kwa kujaza fomu maalum iliyopo kwenye jedwali la ishirini na tatu la Sheria Ndogo hizi na kukubali kulipa faini anayodaiwa.

Kufutwa kwa GN 394

14. Sheria Ndogo hizi zinafuta Sheria Ndogo GN Na. 394 ya tarehe 17/10/2014.

## SEHEMU YA NNE

## JEDWALI

(*Limetungwa chini ya kifungu cha 4(1)*)

### JEDWALI LA KWANZA

1. ADA YA JENGO NA KUKODI MALI YA HALMASHAURI

| Na. | Huduma | Kiwango |
|---|---|---|
| 1 | Nyumba za Halmashauri<br>(a) Kubwa<br>(b) Za kati<br>(c) ndogo | <br>Tsh. 50,000/= kwa mwezi<br>Tsh. 40,000/= kwa mwezi<br>Tsh. 30,000/= kwa mwezi |
| 2 | Ukumbi mkubwa | Tsh. 50,000/= kwa siku |
| 3 | Ukumbi mdogo | Tsh. 30,000/=kwa siku |
| 4 | Viti | Tsh. 500/= kwa kila kiti kwa siku |
| 5 | Masoko yote ya Halmashauri | Tsh. 4,000/= kwa mita za mraba kwa mwezi |
| 6 | Mzunguko wa stendi kuu | Tsh. 4,000/= kwa mita za mraba kwa mwezi |
| 7 | Maeneo Mengine ya Halmashauri | Tsh.4,000/= kwa mita za mraba kwa mwezi |
| 8 | Pango la Chumba | Tsh. 40,000/= kwa mwezi |

| | | |
|---|---|---|
| 9 | Pango la meza la soko | Tsh. 3,000/= kwa mwezi |
| 10 | Huduma ya Choo | Tsh. 200/= @ kila mtu atumiapo |

2. ADA NA USHURU WA MAZAO MCHANGANYIKO

| Na. | Zao | Kiwango |
|---|---|---|
| 1 | Mahindi | 5% kwa gunia la kilo 100 |
| 2 | Maharage | 5% kwa gunia la kilo 100 |
| 3 | Mpunga | 5% kwa gunia la kilo 100 |
| 4 | Mchele | 5% kwa gunia la kilo 100 |
| 5 | Ulezi | 5% kwa gunia la kilo 100 |
| 6 | Karanga | 5% kwa gunia la kilo 100 |
| 7 | Alizeti | 5% kwa gunia la kilo 60 |
| 8 | Muhogo | 5% kwa gunia la kilo 100 |
| 9 | Ngano | 5% kwa gunia la kilo 100 |
| 10 | Matunda | 5% kwa gunia la kilo 100 |
| 11 | Miwa | 5% kwa tripu ya Lori la Tani saba |
| 12 | Mawese | 5% kwa lita 20 |
| 13 | Mazao mengine | 5% ya bei ya kununulia kwa gunia la kilo 100 |

3. ADA YA HUDUMA ZA MACHINJIO, UKAGUZI WA NYAMA NA USHURU WA BUCHA

| Na. | Ada/Ushuru | Kiwango |
|---|---|---|
| 1 | Ada ya Machinjio na Ukaguzi wa nyama kwa kila Ng'ombe atakayechinjwa | Tsh. 4,000/= |
| 2 | Ada ya Machinjio na Ukaguzi wa nyama kwa kila Kondoo na Mbuzi | Tsh 1,500/= |
| 3 | Ada Machinjio na ukaguzi wa nyama kwa kila Nguruwe | Tsh. 2,000/= |
| 3 | 1. Ushuru wa Ngozi ya ng'ombe<br>2. Ushuru wa ngozi ya mbuzi na kondoo | Tsh. 500/=<br>Tsh. 200/= |

4. ADA YA KUENDESHA SHUGHULI ZA UTAMADUNI, BURUDANI NA MICHEZO

*Tangazo la Serikali Na. 29 (Linaendelea)*

| Na. | Ada/Ushuru | Kiwango |
|---|---|---|
| 1 | Kibali cha kuendesha DISCO, Maonesho ya bendi na Sanaa za Maonesho | Tsh.10,000/= kwa siku |
| 2 | Waganga wa Jadi waliosajiliwa | Tsh. 80,000/= kwa mwaka |
| 3 | Pool Table | Tsh. 500/= kwa kila Pool Table kwa siku |
| 4 | Slotting Machine | Tsh. 500/= kwa kila mashine kwa siku |

5. ADA NA USHURU WA VYOMBO VYA USAFIRI KATIKA ENEO LA STENDI NA MAEGESHO YALIYOTENGWA

| Na. | Chombo cha Usafiri | Ushuru wa Maegesho |
|---|---|---|
| 1 | Pikipiki zilizosajiliwa kwa biashara katika maeneo yaliyotengwa | 300/= kwa siku |
| 2 | Teksi | 500/= kwa siku |
| 3 | Lori chini ya Tani saba/pick up/Basi ndogo | 1,000/= kwa siku |
| 4 | Lori zaidi ya Tani saba/ Basi kubwa | 3,000/= kwa siku |
| 5 | Magari mengine yasiyo ya biashara | 500/= kwa siku |

6. ADA NA USHURU WA STENDI

| Na. | Chombo cha Usafiri | Kiwango |
|---|---|---|
| 1 | Teksi/gari dogo chini ya abiria 5 | Tsh. 500/= kwa kutoka kwa siku |
| 2 | Basi chini ya Abiria 25 | Tsh. 1,000/= kwa kutoka kwa siku |
| 3 | Basi zaidi ya Abiria 25 | Tsh. 2,000/= kwa kutoka kwa siku |
| Ada au na Ushuru wa Maegesho ya Vyombo vya Uvuvi ndani ya Nchi na ushuru wa Gati | | |
| 4 | Boti kubwa | Tsh. 2,000/= kwa siku |
| 5 | Boti la Kati | Tsh. 1,000/= kwa siku |
| 6 | Mtumbwi | Tsh. 500/= kwa siku |
| 7 | Gati kupakia na kupakua | Tsh. 1000/= kwa kila tani |

7. ADA NA USHURU WA MAEGESHO YA VYOMBO USAFIRI WA MAJI TOKA NJE YA NCHI, PAMOJA NA USHURU WA MCHANGA TOKA NJE YA NCHI

| NA. | Mtumbwi/Boti | Kiwango |
|---|---|---|
| 1 | Boti Kubwa | Tsh.10,000/=kuingia na kutoka |
| 2 | Boti la Kati | Tsh.7,000/=kuingia na kutoka |
| 3 | Boti Dogo | Tsh.5,000/=kuingia na kutoka |
| 4 | Mtumbwi | Tsh.2,000/=kuingia na kutoka |
| 5 | Mchanga mwambao mwa ziwa Tanganyika | Tsh.2,000/= kwa kila mgeni kutoka nje ya nchi |

8. USHURU WA MADINI YA UJENZI

| Na. | Uzito wa Gari | Kiasi cha Ushuru |
|---|---|---|
| 1 | A. Mchanga<br>1. Tripu moja ya mkokoteni wa Ng'ombe<br>2. Tripu moja ya power tiller<br>3. Tripu moja ya Lori | Tsh. 500/=<br>Tsh. 500/=<br>Tsh. 2,000/= |
| 2 | B. Mawe<br>1. Tripu moja ya mkokoteni wa Ng'ombe<br>2. Tripu moja ya power tiller<br>3. Tripu moja ya Lori | Tsh. 500/=<br>Tsh. 700/=<br>Tsh. 2,000/= |
| 3 | C. Kokoto<br>1. Tripu moja ya mkokoteni wa Ng'ombe<br>2. Tripu moja ya power tiller<br>3. Tripu moja ya Lori | Tsh. 500/=<br>Tsh. 700/=<br>Tsh. 3,000/= |

9. ADA YA MATANGAZO YA BIASHARA

| Na. | Aina ya Tangazo | Kiwango |
|---|---|---|
| 1 | Matangazo yanayong'aa(kwa makampuni ya simu na viwanda) | Tsh. 20,000/= kwa mwezi |
| 2 | Matangazo yanayong'aa (kwa nyumba za kulala wageni) | Tsh. 5,000/= kwa mwezi |

| | | |
|---|---|---|
| 3 | Matangazo yanayong'aa (kwa wafanyabiashara wa kawaida) | Tsh. 3,000/= kwa mwezi |
| 4 | Matangazo yasiyong'aa (kwa wafanyabiashara wa kawaida) | Tsh. 1,000/= kwa mwezi |
| 5 | Matangazo yasiyong'aa (kwa makampuni ya simu na viwanda) | Tsh. 10,000/= kwa mwezi |
| 6 | Matangazo yasiyong'aa (kwa nyumba za kulala wageni) | Tsh. 3,000/= kwa mwezi |
| 7 | Bango la Tangazo linalobadilikabadilika | Tsh. 100,000/= kwa mwezi |
| 8 | Tangazo kwa kutumia kitambaa | Tsh. 3,000/= kwa mwezi |
| 9 | Tangazo kwa kutumia karatasi | Tsh. 1,000/= kwa mwezi |
| 10 | Tangazo kwa kutumia vyombo vya usafiri na vipasa sauti | Tsh. 10,000/= kwa siku |

10. USHURU WA SAMAKI NA DAGAA

| Na. | Aina ya Samaki | Kiwango |
|---|---|---|
| 1 | Samaki wabichi | Tsh. 100 kwa kilo |
| 2 | Samaki wa Mapambo | Tsh. 5,000/= kwa samaki mmoja |
| 3 | Ushuru wa dagaa | Tsh. 15,000/= kwa gunia |
| 4 | Samaki Wakavu:-<br>1. Sanduku kubwa<br>2. Tenga Kubwa<br>3. Tenga la Kati<br>4. Tenga Dogo | <br>Tsh. 15,000/= kwa sanduku<br>Tsh 10,000/= kwa Tenga<br>Tsh. 7,000/= kwa Tenga<br>Tsh. 5,000/= kwa Tenga |

11. USHURU WA SAMAKI NA DAGAA KWENDA NJE YA NCHI

| Na. | Aina ya Samaki | Kiwango |
|---|---|---|
| 1 | Samaki wabichi | Tsh. 150 kwa kilo |
| 2 | Dagaa | Tsh. 20,000/= kwa gunia |
| 3 | Samaki Wakavu:-<br>5. Sanduku kubwa<br>6. Tenga Kubwa<br>7. Tenga la Kati<br>8. Tenga Dogo | <br>Tsh. 20,000/=<br>Tsh.15,000/=<br>Tsh. 10,000/=<br>Tsh. 7,000/= |

12. ADA NA USHURU WA BIDHAA KWENDA NJE YA NCHI

| Na | Aina ya Bidhaa | Kiwango |
|---|---|---|
| 1 | Sabuni | 5% ya bei ya soko |
| 2 | Mafuta ya taa | 5% ya bei ya soko |
| 3 | Disel | 5% ya bei ya soko |
| 4 | Petrol | 5% ya bei ya soko |
| 5 | Mafuta ya kula | 5% ya bei ya soko |
| 6 | Sukari | 5% ya bei ya soko |
| 7 | Nguo | 5% ya bei ya soko |
| 8 | Chumvi | 5% ya bei ya soko |
| 9 | Chuma chakavu | 5% ya bei ya soko |
| 10 | Bidhaa nyingine | 5% ya bei ya soko |

13. ADA YA MAJENGO, UPIMAJI WA ARDHI NA VIBALI VYA UJENZI

| Na. | Ada ya kibali cha ujenzi na ukaguzi wa ramani | kiwango |
|---|---|---|
| 1 | Jengo la makazi | Tsh. 15,000/= |
| 2 | Jengo la makazi la ghorofa moja | Tsh. 30,000/= |
| 3 | Jengo la makazi zaidi ya ghorofa moja | Tsh. 50,000/= |
| 4 | Jengo la makazi na biashara | Tsh. 20,000/= |
| 5 | Jengo la biashara | Tsh. 25,000/= |
| 6 | Jengo la biashara zaidi ya ghorofa moja | Tsh. 70,000/= |
| 7 | Jengo la kiwanda kidogo na ghala | Tsh. 50,000/= |
| 8 | Jengo la kiwanda/kituo cha mafuta | Tsh. 150,000/= |
| 9 | Jengo la taasisi ya dini, NGO, Chama cha Siasa | Tsh. 20,000/= |
| 10 | Jengo la taasisi ya dini, NGO, Chama cha Siasa | Tsh. 50,000/= |
| 10 | Ada za Maombi ya Upimaji na Utumiaji wa Ardhi<br>1. Maombi ya Kiwanja/ Ardhi<br>2. Ada ya malipo ya awali ya kiwanja/ Ardhi (Premiun) | <br><br>Tsh. 10,000/=<br>7.5% ya thamani ya Ardhi |

14. USHURU WA MAZAO YA MALIASILI

| Na. | Aina ya Maliasili | Kiwango |
|---|---|---|
| 1 | Mbao za mninga | Tsh. 2,000/= kwa kila ubao |
| 2 | Mbao za mkaratusi | Tsh. 1,000/= kwa kila ubao |
| 3 | Mbao nyinginezo | Tsh. 1,000/= kwa kila ubao |
| 4 | Gogo kubwa | Tsh. 5,000/= kwa kila gogo |
| 5 | Gogo la kati | Tsh. 3,000/= kwa kila gogo |
| 6 | Gogo dogo | Tsh. 2,000/= kwa kila gogo |
| 7 | Mkaa | Tsh. 2,000/= kwa kila gunia |
| 8 | Kuni | Tsh. 5,000/= kwa tani moja |
| 9 | Asali | Tsh. 200/= kwa lita |
| 10 | Nta | Tsh. 500/= kwa kilo |

15. ADA NA USHURU WA MASOKO NA MINADA

| Na. | Bidhaa | Kiwango |
|---|---|---|
| 1 | Ada na Ushuru wa bidhaa sokoni kwa meza | Tsh. 200/= kwa siku |
| Ada na Ushuru wa Minada | | |
| 2 | Meza | Tsh. 1,000/= kwa siku |
| 3 | Wauza mitumba/nguo | Tsh. 1,000/= kwa siku |
| 4 | Mamantilie | Tsh. 500/= kwa siku |
| 5 | Wauza soda | Tsh. 1,000/= kwa siku |
| 6 | Wauza bia | Tsh. 2,000/= kwa siku |
| 7 | Biashara ndogondogo | Tsh. 500/= kwa siku |
| 8 | Pombe za asili | Tsh. 1,000/= kwa siku |
| Ada na Ushuru wa Mifugo Mnadani | | |
| 9 | Ng’ombe | Tsh. 5,000/= kwa kila mmoja |
| 10 | Mbuzi/Kondoo/Nguruwe/ na Punda | Tsh. 1,500/= kwa kila mmoja |
| 11 | Kuku/Kanga na Bata | Tsh. 1,000/= kwa kila mmoja |

16. ADA YA KIBALI CHA KUNUNUA MAZAO YA KILIMO

| Na. | Idadi ya Gunia | Kiwango kwa safari moja |
|---|---|---|
| 1 | Gunia 1- 100 | Tsh.20,000/= |
| 2 | Gunia 100 - 500 | Tsh. 80,000/= |
| 3 | Gunia 500 - 1000 | Tsh. 150,000/= |

| | | |
|---|---|---|
| 4 | Gunia 1,000 -1,500 | Tsh. 200,000/= |
| 5 | Gunia 1,500 - 2,000 | Tsh. 250,000/= |
| 6 | Gunia 2,000 - 3,000 | Tsh. 300,000/= |
| 7 | Gunia zaidi ya 3,000 | Tsh. 500,000/= |

17. ADA NA USHURU WA MIFUGO INAYOSAFIRISHWA KWENDA NJE YA NCHI

| NA. | MIFUGO | KIWANGO |
|---|---|---|
| 1 | Ng'ombe | Tsh. 10,000/= |
| 2 | Punda | Tsh. 10,000/= |
| 3 | Farasi | Tsh. 10,000/= |
| 4 | Mbuzi | Tsh. 5,000/= |
| 5 | Kondoo | Tsh. 5,000/= |
| 6 | Nguruwe | Tsh. 5,000/= |
| 7 | Bata | Tsh. 1,000/= |
| 8 | Kanga | Tsh. 1,000/= |
| 9 | Kuku | Tsh. 500/= |

18. ADA NA USHURU WA MAZAO MCHANGANYIKO YANAYOSAFIRISHWA NJE YA NCHI

| Na. | Zao | Ada | Ushuru |
|---|---|---|---|
| 1 | Mahindi | 10% | 10% |
| 2 | Maharage | 10% | 10% |
| 3 | Mpunga | 10% | 10% |
| 4 | Mchele | 10% | 10% |
| 5 | Ulezi | 10% | 10% |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 6 | Karanga | 10% | 10% |
| 7 | Alizeti | 10% | 10% |
| 8 | Muhogo | 10% | 10% |
| 9 | Ngano | 10% | 10% |
| 10 | Matunda | 10% | 10% |
| 11 | Miwa | 10% | 10% |
| 12 | Mawese | 10% | 10% |
| 13 | Mazao mengine | 10% | 10% |
| 14 | Ufuta | 10% | 10% |
| 15 | Tumbaku | 10% | 10% |
| 16 | Mikambaa | 10% | 10% |
| 17 | Mazao mengine | 10% | 10% |

19. USHURU WA HUDUMA

| Na. | Aina ya huduma | KIWANGO |
|---|---|---|
| 1 | Zuku | 0.3%kwa mwaka |
| 2 | Azam | 0.3%kwa mwaka |
| 3 | Continental | 0.3%kwa mwaka |
| 4 | Minara ya simu | 0.3%kwa mwaka |
| 5 | Vituo vya kuuzia mafuta | 0.3%kwa mwaka |
| 6 | Runinga ya nyaya (Cable) | 0.3%kwa mwaka |
| 8 | TANESCO | 0.3%kwa mwaka |
| 9 | TTCL | 0.3%kwa mwaka |
| 10 | BENKI YA NMB | 0.3% kwa mwaka |
| 11 | BENKI YA CRDB | 0.3% kwa mwaka |
| 12 | BENKI YA POSTA | 0.3%kwa mwaka |
| 13 | TUNAKOPESHA LTD | 0.3%kwa mwaka |
| 14 | BAYPOT | 0.3%kwa mwaka |
| 15 | ABC | 0.3%kwa mwaka |
| 16 | PLATINUM | 0.3% kwa mwaka |
| 17 | TING | 0.3% kwa mwaka |
| 18 | DSTV | 0.3% kwa mwaka |

## JEDWALI LA PILI

*(Limetungwa chini ya kifungu cha 5)*

1. MASOKO YALIYOTAMBULIWA NDANI YA HALMASHAURI

2. Soko kuu Namanyere 12. Soko la Lyazumbi

3. Soko la Kirando
4. Soko la Kamwanda
5. Soko la Kabwe
6. Soko la Ntanganyika
7. Soko la Korongwe
8. Soko la Chala
9. Soko la Kipande
10. Soko la Wampembe
11. Soko la Kantawa
12. Soko la Mtenga
13. Soko la Mpasa
14 .Soko la Uwanja wa Ndege
15 .Soko la Tanamakunda
16 .Soko la Mashete
17 .Soko la Isale
18 .Soko la Ntatumbila
19 .Soko la Jumamosi la Kasawanga
20 .Soko la Lunyala
21 .Soko la Misunkumilo

2. MAGULIO YANAYOTAMBULIWA RASMI NDANI YA HALMASHAURI KUWA NDIYO MAENEO AMBAYO WAFANYABIASHARA WANATAKIWA KUTOZWA USHURU NA ADA.

| NA. | KATA | NA. | VITUO VIKUBWA | VITUO VIDOGO VYA MASOKO |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Namanyere | 1 | Soko la mazao la kimataifa Isunta | Kanazi, |
| 2 | Kipundu | | | Kakoma, Mbwendi |
| 3 | Nkomolo | | | Lunyala, Mkole, Ipanda |
| 4 | Majengo | | | |
| 4 | Isunta | | | |
| 5 | Isale Asilia | 2 | Isale Godown | Msilihofu, Mtapenda |
| 6 | Isale | 3 | Ntuchi Godown | Kitosi, Ifundwa |
| 7 | Kate | 4 | Kate Godown | Nkata, Itekesya, Nchenje |
| 8 | Sintali | 5 | Nkana Godown | Sintali, Nkomanchindo, Kasapa |
| 9 | Myula | 6 | Ntalamila Godown | Chonga, Chalatila, Myula |
| 10 | Kipande | 7 | Kantawa Godown | Nkundi, Kipande, Kalundi, Nkomolo II |
| 11 | Nkandasi | 8 | Kasu Godown | Katani, Milundikwa, Kisula, Malongwe |
| 12 | Mkwamba | 9 | Swaila Godown | Tambaruka, Lyele, Itindi |
| 13 | Chala | 10 | Chala Godown | - |
| 14 | Ntatumbila | 11 | Ntatumbila Godown | Kacheche, londokazi |
| 15 | Machete | 12 | Machete Godown | Miombo |
| 16 | Mtenga | 13 | Mtenga Godown | matala |
| 17 | Paramawe | 14 | Paramawe Godown | Kizi, Lyazumbi |
| 18 | Kabwe | 15 | Kabwe | |
| 19 | Korongwe | 16 | Korongwe | Utinta, Kazovu |
| 20 | Kirando | 17 | Kamwanda Godown | |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 21 | Itete | | | Chongokatete |
| 22 | Kipili | 18 | Kipili | Katongolo, Mandakerenge |
| 23 | Mkinga | 19 | Mkinga | |
| 24 | Ninde | 20 | Namansi | Ninde |
| 25 | Kizumbi | 21 | Kizumbi | Ngundwe |
| 26 | Wampemb e | 22 | Wampembe | Izinga, Mwinza |
| 27 | Kala | 23 | King'ombe | Kilambo, Kala, Mlambo. |
| | | 24 | Mpasa | |

3. MASOKO YA SAMAKI NA DAGAA

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1 | Mwalo wa Kabwe | 8 | Mwalo wa Mkilinga |
| 2 | Soko la Korongwe | 9 | Mwalo wa Mpasa |
| 3 | Mwalo wa Kirando | 10 | Mwalo wa Lyele |
| 4 | Malo wa Ntanganyika | 11 | Mwalo wa Kizumbi |
| 5 | Mwalo wa Namansi | 12 | Mwalo wa Wampembe |
| 6 | Mwalo wa Ninde | 13 | Mwalo wa Kala |
| 7 | Mwalo wa Msamba | 14 | Mwalo wa Lupata |
| | | 15 | Mwalo wa Kapumpuli |

JEDWALI LA TATU.

HATI YA KUFIFILISHA KOSA

*(Limetungwa chini ya kifungu cha 15)*

Mimi ………………………………..nakiri mbele ya …………………………….ambaye ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Nkasi, kwamba mnamo tarehe……………….. ya mwezi……………mwaka ……………..nilitenda kosa la kukiuka masharti ya kifungu cha……………… cha Sheria Ndogo za Halmashauri ya Wilaya ya Nkasi (Ada na Ushuru) za Mwaka 2016.

Na kwa Mamlaka aliyopewa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri, Niko tayari kulipa kiasi cha Ada/Ushuru ninaodaiwa pamoja na faini.

NATHIBITISHA KWAMBA MAELEZO HAPO JUU NI YA KWELI NA NIMEYATOA KWA HIARI YANGU KADRI YA UFAHAMU WANGU

Leo tarehe …………ya mwezi …………………… mwaka …………………
Jina …………………………………sahihi …………………………………

Mbele ya
Jina ……………………………………………….
Cheo ………………………………………………
Saini ……………………………………………….

JEDWALI LA NNE
*(Limetungwa chini ya kifungu cha 6(6))*

MAOMBI YA KIBALI CHA KUNUNUA MAZAO KATIKA MASOKO YA HALMASHAURI YA WILAYA YA NKASI

SEHEMU ‘A’

(Ijazwe na mwombaji)

1. Jina la kampuni/Shirika/Ushirika/Mnunuzi ……………………………..

2. Anuani yake S. L. P ……………………Simu ………………Wilaya …….
3. Mahali ofisi yake ilipo………………….mji ………………….. mtaa ……
4. Mahalianapoishi/Mji……………………………………………………

5. Namba ya Leseni ya Ununuzi wa mazao ………………………………
6. Namba ya kuandikishwa Shirika/Kampuni…………………………………
7. Mazao anayotaka kununua …………………………………………….
8. Kiasi anachotaka kununua Gunia/Kgms………………………………….
9. Masoko/kijiji atakaponunulia ………………………………………….
10. Maghara atakayotumia kusombea mazao yake …………………………..

NATHIBITISHA: Kuwa maelezo yote niliyotoa hapo juu ni sahihi na kweli.

1. Jina la mwombaji ………………………………………………….
2. Sahihi ya mwombaji ……………………………………………….
3. Mhuri ……………………………………………………………
4. Tarehe ……………………………………………………………..

Nakala ya kibali kwa ajili ya ukaguzi wakati wowote:

Nakala ya kibali hiki itabaki kwa:-

- Mkurugenzi Mtendaji Wilaya (W) …………………………….
- Afisa Mtendaji Kijiji cha ………………………………………

………………………………...
MKURUGENZI MTENDAJI (W)
Halmashauri ya Wilaya ya Nkasi

Nembo ya Halmashauri ya Wilaya ya Nkasi ilibandikwa kwenye Sheria Ndogo hizi kwa kufuata Azimio lililopitishwa kwenye mkutano wa Halmashauri uliofanyika tarehe 27 mwezi Aprili mwaka 2016. Mbele ya:-

JULIUS MSELECHE KAONDO,
*Mkurugenzi Mtendaji*
*Halmashauri ya Wilaya ya Nkasi.*

SUMUNI ZENO MWANAKULYA,
*Mwenyekiti*
*Halmashauri ya Wilaya ya Nkasi.*

NAKUBALI,

Dodoma,
09 Januari, 2017

GEORGE B. SIMBACHAWENE (MB)
*Waziri wanchi-or-Tamisemi*